# MSUMENO WA WIMA NA MLALO

PANDA MITI KIBIASHARA
PRIVATE FORESTRY PROGRAMME

## Taarifa za jumla

- Misumeno hii maalumu imebuniwa ili kukidhi kutumika kirahisi kwa kuzingatia ukubwa wa magogo na aina za miti.
- Mitambo hii inaweza kutumika kuchana/kupasua aina yoyote ya mbao, laini au magumu
- Mashine hii inayo fremu ngumu pamoja na nguzo mbili iliyobuniwa maalumu kuhimili kazi ngumu ya muda mrefu ya kuchana mbao.
- Msumeno unayo magurudumu mawili yanayotembeza msumeno na yenye uwiano mzuri wa usawa yaliyofungwa kwenye mkanda wenye magurudumu (bearings) na ulio na mfuniko wa kuzuia vumbi.
- Msumeno umewekewa uzio wa chuma unaoulinda na kwa usalama wa watumiaji
- Unapoendeshwa ipasavyo na kupasua mbao kwa usahihi mnyororo huu unawezesha udhibiti wa upotevu wa mbao kwa asilimia 55-70.
- Aina hii ya mashine inahitaji ujuzi wa uhakika katika kupasua mbao.
- Mtambo huu umefungwa jeki pamoja na jiliwa yenye skurubu (screw vices) kwa ajili ya kushikilia magogo




## Vipimo na taarifa za matengenezo

- Msumeno unauwezo wa kupasua meta za ujazo 15 kwa zamu (endapo waendeshaji 6 watafanya kazi kwa saa 8)
- Urefu wa reli ya msumeno wa mlalo ni meta 18, ambao unatumia toroli la urefu wa meta 4. Mashine yake inaupana wa meta 3 katika sehemu pana zaidi. Urefu wake wa mwisho kabisa ni meta 2.
- Msumeno wa wima una urefu wa meta 2, wenye meza ya ukubwa wa sentimeta 104x107.
- Uzito wa msumeno wa mlalo ni kilo 2,500, wakati uzito wa msumeno wa wima ni kilo 1,400.
- Uwezo wa kupasua mbao kwa maana ya urefu ni sentimeta 95, pamoja na uwezo wa mwisho wa kupasua kwa kina cha kipenyo cha sentimeta 100.
- Kisu cha kuchania mbao kwa ,msumeno wa wima kinaurefu wa futi 31 (inakadiriwa kuwa na meta9.5) na urefu wa kisu cha msumeno wa wima ni futi 24 (inakadiriwa kuwa meta 7.5). Visu vyote viwili vinaweza kutumia visu vyenye ukubwa wa inchi 2.5-3. Upana wa visu uwe wa milimita 1.1.
- Msumeno wa mlalo unakasi ya kuzunguka mara 600 kwa dakika na ule wa wima unakasi ya kuzunguka mara 500 kwa dakika.
- Umeme unaohitajika kwa msumeno wa mlalo ni 15 kWh na 10 kWh kwa msumeno wa wima. Mashine lazima irekebishwe na iwe na uwiano mzuri baada ya kufungwa. Beringi zichunguzwe kila baada ya miezi mitatu na zibadilishwe inapohitajika.







## Taarifa za ununuaji/manunuzi

- Misumeno hii ni ile ya gharama ndogo kwa ajili ya viwanda vya kupasua mbao.
- Misumeno ya mikanda inaweza kununuliwa toka nchi nyingi (kwa mfano China, India, Africa ya kusini).
- Gharama zifuatazo hutokea wakati wa manunuzi ya mashine hizi:
  - Bei ya kununlia (inayojumuisha usafirishaji na bima) kwa msumeno kamba wa mlalo: Euro 5,900 na msumeno kamba wa wima: Tsh 8,840,000 (3,200 EUR) .
  - Kodi ya kuiningiza nchini: 27 %
  - Kodi ya ongezeko la thamani kwa kununua na kuingiza nchini: 18 %
  - Gharama za kutoa mzigo bandarini pamoja na gharama za bandari Euro 3,600 kwa msumeno kamba wa mlalo na Euro 1,800 kwa msumeno kamba wa wima.
  - Gharama za usafirishaji: Euro 450 kwa msumeno kamba wa mlalo na Euro 350 kwa msumeno kamba wa wima.
- Mambo ya kuzingatia wakati wa kununua masshine:
  - Uwezo wa mashine
  - Upatikanaji wa vipuli na waendeshaji waliobobea
  - Hati ya udhamini wa kurudisha mashine
  - Utaratibu wa matengenezo ya mashine

## Makadirio ya gharama-faida

| Maelezo | Msumeno kamba wa mlalo | Msumeno kamba wa wima |
|---|---|---|
| Uendelevu | Mbao zilizochanwa na uzalishaji mdogo wa samani na bidhaa za kuunganishwa. | |
| Gharama za uwekezaji | TSH 34,680,000 (12,550 EUR) | TSH 12,790,000 (6,800 EUR) |
| Idadi ya waendeshaji | 3 | 3 |
| Umeme | 15 kWh (wastani wa 11,25 kWh) | 10 kWh (wastani wa 7,5 kWh) |
| Gharama za umeme (kwa mwezi, kwa kuzingatia awamu moja ya masaa 8, katika siku 5 za kazi | 630,000 TSH | 420,000TSH |
| Matengenezo | Kila siku: (Kabla ya kuwasha mashine ): tazama na ukase misumeno kamba, vilainishi na bearing, safisha eneo la kuchaia mbao, kunoa visu, (vifaa vinavohitajika: mashine ya kunolea, vilainishi. Kwa mwezi: Funga beringi, tazama sukepindi (coil) Vipuli hitajika: Beringi,misumeno, Mita ya mkazo (tension meter) sukepindi (coil) | |
| Gharama za matengenezo kwa mwezi (kwa mfumo mzima) | 72,000 TSH (wafanyakazi), 80,000 TSH (vipuli), 400,000 TSH (Kunoa msumeno) | |
| Kiwango cha juu cha uzalishaji kwa mwaka | Mita za ujazo 3,600 | |

## Huduma za kituo zinazohusiana na kituo cha mafunzo

- Kupima sampuli za mbao za mteja.
- Huduma za maelezo kwa wadau na wateja wenye lengo la kununua.
- Huduma za ushauri wadau na wateja wenye lengo la kununua.
- Mafunzo kwa wamiliki wa viwanda, mameneja na waendeshaji juu ya matumizi ya
- Mafunzo juu ya upasuaji sahihi wa mbao na namna ya kupunguza uharibifu wa mbao. (recovery rete).

## Mawasiliano na namna ya kufika kituoni

Kituo cha Mafunzo ya Viwanda vya Mazeo ya Misitu (KMVMM)

Kinyanambo

Mafinga

Mr. Edigary, Mwaifweya Meneja wa Kituo.

Barua pepe: edigary.mwaifweya@privateforestry.or.tz

Tel: +255 744 874 521

Maelezo kwa watumiaji magari: Njia panda ya kituo cha Mafuta cha CF, barabara iendayo Madibira, endesha umbaki wa kilomita moja. Utaona kibao cha kituo upande wa kushoto mwa barabara, mkabala na kiwanda cha mkaa.

## Kuhusu Programu ya Panda Miti Kibiashara PFP)

Pandamiti Kibiashara husaidia umiliki binafsi wa mashamba ya miti hasa katika uanzishwaji na utunzaji wa mashamba ya miti kwa wakulima wadogo, kadhalika viwanda vya mazao ya misitu pamoja na ukuaji wa soko la mazao ya mbao yaliyokomaa ambayo yatanufaisha wadau wote. Programu inatekeleza katika Mikoa minne: Iringa, Njombe, Morogoro na Ruvuma.

Mradi unafadhiliwa na Wizara ya Mambo ya Nje ya Finaland na Wizara ya Maliasili na Utalii ya Tanzania.

United Republic of Tanzania
MINISTRY OF NATURAL RESOURCES AND TOURISM
Forestry and Beekeeping Division

FORMIN.FINLAND.FI
MINISTRY FOR FOREIGN AFFAIRS OF FINLAND

© Private Forestry Programme 2018